

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA SABA

27 APRILI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA SABA – TAREHE 27 APRILI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA KILIMO:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

WAZIRI WA MADINI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

191. MHESHIMIWA ENG. CHACHA MWITA WAMBURA (GEITA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, upi mkakati wa kuunda ajira na kukuza uchumi wa Vijana kupitia Miradi ya uzalishaji na ujasiriamali ili kupunguza utegemezi wa Sekta ya madini – Geita.

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

192. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni haja ya kutenga sehemu ndogo ya fedha za Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya samani za Ofisi na ufuatiliaji wa miradi ya Mfuko huo.

193. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali imejipangaje kumaliza tatizo la Matundu ya Vyoo katika Halmashauri nchini.

194. MHESHIMIWA JUMA MUSTAFA KAWAMBA (IGAGULA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Shule za Msingi na Sekondari pamoja na miundombinu katika Shule zilizopo Jimbo la Igalula.

195. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (TABORA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko la Kisasa la Machinga katika Jimbo la Tabora Mjini.

196. MHESHIMIWA ANNE KILANGO MALECELA (SAME MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Barabara ya Hedaru - Mamba Vunta yenye Km 42.44 itaboreshwa ili kuokoa uchumi wa Wananchi wa Kata ya Mamba Vunta.

WIZARA YA NISHATI:

197. MHESHIMIWA ENG. JOHNSTON JOHANSEN MUTASINGWA (BUKOBA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itakamilisha upanuzi wa Kituo cha umeme Kibeta.

WIZARA YA FEDHA:

198. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, kwa nini Serikali haitoi bei elekezi kwa makato ya huduma za *Mobile Money* ili kuwapunguzia gharama Wananchi.

WIZARA YA MAJI:

199. MHESHIMIWA YAGI MAULID KIARATU (SINGIDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa Maji unaotekelezwa katika Mitaa 38 ya Manispaa ya Singida utakamilika ili Wananchi wapate huduma ya maji safi na salama.

**200. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO
(TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria utakamilika na kutoa huduma ya Maji kwa Mitaa yote 81 ndani ya Mji wa Tarime.

WIZARA YA KILIMO:

**201. MHESHIMIWA COSMAS MTESIGWA BULALA
(KWIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa ghala la kuhifadhia Mazao katika Kijiji cha Hungumalwa.

202. MHESHIMIWA ENOCK ZADOCK KOOLA (VUNJO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaanzisha Kituo cha kukodi vifaa vya kilimo katika Wilaya ya Moshi Vijijini.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MADINI

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

DODOMA
27 APRILI, 2026

BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE

